Tanzania yang'ara DStv Eutelsat Star Awards

Jumatano, Machi 06, 2019 — updated on Februari 16, 2021



Muktasari:

Kwa mara nyingine tena Tanzania imeibuka kinara katika tuzo za kimataifa za wanafunzi zijulikanazo kama DStv Eutelsat Star Awards baada ya mwanafunzi Priscilla Marealle kutoka Sekondari ya St. Mary Goreti mkoani Kilimanjaro kushinda tuzo ya ubunifu wa bango la elimu ya anga.

Dar es Salaam. Mwanafunzi Priscilla Marealle (19) kutoka shule ya sekondari ya St Mary Goreti, Kilimanjaro amepeperusha bendera ya Tanzania kwa kunyakua nafasi ya kwanza katika kipengele cha uchoraji bango la elimu ya anga

Captured October 30, 2026 from https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/tanzania-yang-ara-dstv-eutelsat-star-awards-2957576 (page 1 of 3)

miongoni mamia ya wanafunzi kutoka zaidi ya nchi zaidi ya 10 barani Afrika.

Katika tuzo hizo zijulikanazo kama DStv Eutelsat Star Awards uhusisha uandishi wa insha maalumu au kuandaa mabango yenye ujumbe kuhusiana na elimu ya anga hususan setelaiti, hushirikisha wanafunzi wote wa sekondari wenye umri kati ya miaka 14 na 19 ndani ya bara la Afrika.

Katika msimu huu wa nane, washindani walitakiwa kuandika insha au kubuni bango litakaloelezea ni namna gani setelaiti zinaweza kutumika zaidi ili kuleta maendeleo chanya ulimwenguni.

ALSO READ

Sh70 milioni kuinua wakulima wa mwani Mtwara



Biashara 44 min ago

Jumuiya za kiraia zafikia maazimio manane kuimarisha umoja na amani



Kitaifa 44 min ago

“Nimefurahi sana kupokea taarifa hizi nzuri. Naamini ushindi wangu utakuwa ni chachu kwa wanafunzi wenzangu nchini kujitokeza kwa wingi na kushiriki katika tuzo kama hizi na mashindano mengine ya kitaaluma ya ndani na nje ya nchi, ndoto huanza kufanya kazi pale unapojiamini,” alisema Priscilla.

(AD)

Naye Mkuu wa Uhusiano wa MultiChoice Tanzania Johnson Mshana, alisema huu ni msimu wa tatu mfululizo kwa Tanzania kuendelea kung’ara katika tuzo hizi ambazo mwaka

huu zimefanyika Accra nchini Ghana na jopo la majaji liliongozwa na Paolo Nespoli, mwanaanga nguli kutoka European Space Agency (ESA).

“Tulianza kupeperusha bendera yetu na kijana Davids Bwana msimu wa sita baada ya kushika nafasi ya pili Afrika katika kipengele cha uandishi wa insha, kisha tukaibuka kidedea baada ya kupokea taarifa za ushindi wa kwanza wa kijana Taheer Rashid katika msimu wa saba mwaka jana na leo hii tunayo furaha kubwa kuona kuwa tumeendeleza wimbi la ushindi,” alisema.

Alisema pamoja na kupata cheti, Pricilla atapata fursa yeye na mzazi au mlezi kutembelea Kituo cha Anga cha Afrika Kusini na pia kutembelea makao makuu ya MultiChoice jijini Johannesburg kama mgeni maalumu wa DStv huku shule aliyotoka ikipata zawadi ya cheti na kufungiwa huduma ya DStv bure.

Aidha kwa upande wa uandishi wa insha kijana Tanaka Chonyera kutoka nchini Botswana aliweza kujinyakulia ushindi wa kwanza.

Captured October 30, 2026 from https://www.mwananchi.co.tz/mw/habari/kitaifa/tanzania-yang-ara-dstv-eutelsat-star-awards-2957576 (page 3 of 3)